

Hati ya upatikanaji kwa ajili ya Kisukari aina ya kwanza

Dunia nzima leo, watu wenye kisukari aina ya kwanza wanakufa kwasababu wanashindwa kununua au kupata insulini, elimu na tiba.

Kujiokoa na kuishi vizuri, kila mwenye kisukari aina ya kwanza ana haki zifuatazo:

1. Haki ya kuwa na insulini

Kila mmoja anatakiwa kuwa na insulini na sindano za kutosha.

2. Haki ya kujua kiwango cha sukari kwenye damu

Kila mmoja anatakiwa aweze kupima kiwango cha sukari kwenye damu kila mara.

3. Haki ya kupata elimu ya kisukari

Kila mmoja anatakiwa kuelewa hali yake, ikiwa ni pamoja na kurekebisha dozi ya insulin.

4. Haki ya matibabu

Kila mmoja apate matibabu hospitalini katika dharula na mwendelezo wa matibabu ya kibingwa kutoka kwa mtu anayeelewa vizuri kisukari.

5. Haki ya kuishi bila kubaguliwa

Mtu yeyote asioneshewe ubaguzi wa aina yeyote kwa sababu ana aina ya kwanza ya kisukari.

MAELEZO MAFUPI YA HATI

1. Haki ya kuwa na insulini

Hii inamaanisha kushushwa kwa bei, upatikanikaji kwa wingi, na insulini ya kutosha kuweka sukari katika damu sawa iwezekanavyo.

2. Haki ya kujua kiwango cha sukari kwenye damu

Kila mtu mwenye kisukari aina ya kwanza anatakiwa kuwa na katika hali ya kawaida, mashine na vijiti vya kupimia damu, sindano za glukagoni kwa dharula na vijiti vya mkojo vya kitoni.

Kila mmoja awe na uwezo wa kupata sindano ya glukagoni akipata sukarisukatiti ya hatari. Waweze pia kupima kitoni inayotokea wakati sukari iko juu na ni hatari isiposhughulikiwa. Kiasi cha njiti za kupimia ziwepo na kupatikanika. Hii inamaanisha mtu aweze kupima kiwango cha sukari katika damu angalau mara nne kwa siku.

3. Haki ya kupata elimu ya kisukari

Kupata elimu ya kisukari kwa kila mmoja mwenye kisukari aina ya kwanza ni muhimu ili waweze kutambua hali yao. Kama mtu mwenye kisukari aina ya kwanza atapata insulini na vifaa, ila hawajui kutumia vifaa na dawa, wanakua bado hatarini. Kuelewa jinsi insulini inavyofanyakazi, vitu vinavyoharibu kiwango cha sukari katika damu, na jinsi ya kutibu ikiwa juu au ikiwa chini ni muhimu kwa afya ya mtu mwenye kisukari aina ya kwanza.

4. Haki ya matibabu

Kila mmoja apate matibabu bora wakati wa kugundulika kutoka kwa mtu aliebobe na anayeelewa kisukari aina ya kwanza. Wanatakiwa pia kupata mwendelezo wa tarehe na ushauri toka kwa wahudumu bobezi wa afya. Kama mtu mwenye kisukari akijikuta katika hali ya dharula kunatakiwa matibabu kwao. Wakipata matatizo nyemelezi, wapate ushirikiano toka kwa madaktari bingwa kuhakikisha anatibiwa ipasavyo.

5. Haki ya kuishi bila kubaguliwa

Sehemu nyingi watu wenye kisukari aina ya kwanza wanazuiliwa kupata ajira. Wanawake wanaonekana hawafai kuolewa na kupata watoto. Kila mmoja mwenye kisukari aina ya kwanza ana haki ya kuajiriwa, kuoja/ kuolewa na sio kuhukumiwa na kuonwa ni dhaifu.

Nani anaweza kuweka sahihi?

Mtu yeyote na shirika lolote wanaweza kuweka sahihi.

HATI hii itatumika kufanya nini?

HATI itatumika kuongeza juhudi katika kutangaza sukari aina ya kwanza dunia nzima. Itaionesha Dunia kua kuna sauti nyingi zilizoungana kwa haki hii. Inaweza kutumika kubadilisha maamuzi ya serikali na mashirika ili sera zibadilishwe na haki ya mtu mwenye aina ya kwanza ya sukari ipewe kipaumbele.

Nini maana ya “upatikanaji”

Kwetu, upatikanaji unamaanisha garama za ununuaji wa bidhaa hauathiri uwezo wa kulipia huduma muhimu nyingine kama chakula, malazi na elimu. Hali ya kiafya isiwe kitisho kwa maisha.

MADA

Sukarisukatiti ni upungufu wa sukari katika mzunguko wa damu, au hujulikana zaidi kama sukari ilioshuka kwenye damu.

Sindano ya glukagoni ni dawa ya dharula inayotumika kutibu sukarisukatiti ya hatari kwa mgonjwa mwenye kisukari aliepoteza fahamu au hawezi kula sukari kwa njia ya mdomo.

Mashine ya sukari ni kifaa kinachopima wingi wa sukari katika damu.

Vijiti ya kupimia kitoni, hutumika kuangalia kitoni katika mkojo. Bila insulini ya kutosha, seli za mwili haziwezi kuchukua sukari na hubaki katika hali ya njaa, huvunja mafuta kwa ajili ya nguvu.

Kitoni ni zao litokanalo na kuvunjwa kwa mafuta, kiwango kikubwa cha hio katika damu inaweza kua sumu.